# TNMC Habari

Toleo NO. 011

TOLEO MAALUMU AGOSTI, 2024

HALIUZWI www.tnmc.go.tz @tnmchabari


# Waziri Mhagama Asisitiza Kauli Nzuri Kwa Wateja, Uwajibikaji, Weledi Kwa watumishi wa Afya.



- *Rasmi Akabidhiwa Ofisi na Mtangulizi Wake*

**"Kauli Nzuri" kwa wagonjwa ni tiba namba moja ambayo inamsaidia mgonjwa"**

*-Mhe. Mhagama*

Uk 01

## Msajili TNMC: Mkazingatie Maadili ya Taaluma ya Uuguzi na Ukunga.

Uk 03





**Watahiniwa 3099 wafanya Mtihani wa Usajili na Leseni** Uk 02

# Waziri Mhagama asisitiza Kauli Nzuri Kwa Wateja, Uwajibikaji, Weledi kwa watumishi wa Afya



**Na Mwandishi wetu**

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama amewasisitiza watumishi wa sekta ya Afya nchini kuzingatia kauli nzuri, uwajibikaji na weledi wakati wa utoaji wa huduma kwa wananchi.

Waziri Mhagama ameyasema hayo Agosti 16, 2024 katika Ofisi za Wizara Afya zilizopo Mji wa Serikali, Mtumba Jijini Dodoma baada ya kukabidhiwa ofisi na aliyekuwa Waziri wa Wizara Afya Mhe. Ummy Mwalimu.

***"Kauli nzuri kwa wagonjwa ni tiba namba moja ambayo inamsaidia mgonjwa kwa asilimia 30 au zaidi kwa hivyo nasisitiza kutumia kauli nzuri kwa wagonjwa."*** Amesema Waziri Mhagama.

Katika hatua nyingine, akizungumza na Menejimenti pamoja na watumishi wa Sekta ya Afya baada ya kukabidhiwa ofisi, Mhe. Jenista, amesisitiza umuhimu wa kuhakikisha mifumo yote inayosaidia wakati wa utoaji huduma kwa wagonjwa inawasiliana kuanzia kwenye ngazi ya Zahanati hadi Hospitali za Rufaa ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

***"Tunawenzetu ambao wana simamia Afya msingi na wengine tunaendelea huku juu lakini Mtanzania anaetibiwa kwenye Afya msingi na huku juu ni huyohuyo mmoja, tufikie mahali mgonjwa akitibiwa kwenye Zahanati Mganga wa Hospitali ya Wilaya awe anajua kuwa kuna mgonjwa anatibiwa kwenye Zahanati lakini kwa ugonjwa huo hawezi kupata huduma hiyo kwenye Zahanati."*** Amesema Mhe. Mhagama

Kwa upande wake aliyekuwa Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu, akimkabidhi Ofisi, amempongeza Mhe. Jenista Mhagama kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa Waziri wa Afya.

***"Umekuwa Kiongozi mwenye uzoefu wa kutosha ndani ya Serikali, naamini kwa uwezo wako pamoja na timu hii ya Wizara unaweza kuendelea zaidi katika kuboresha Sekta ya Afya nchini"*** *amesema Mhe. Ummy.*

Naye, Mhe. Jenista amempongeza Mhe. Ummy Mwalimu kwa uongozi wake ndani ya Wizara ya Afya kwa kipindi chote alichofanya kazi ndani ya Sekta ya Afya kwa miaka 14.



Viongozi wengine wageni walioshiriki kwenye shughuli hiyo ni Naibu Katibu Mkuu Bw. Ismail Rutamila, Dkt. Irene Isaka, Mkurugeni Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima Kwa Pamoja wameahidi kutoa ushirikiano kwa Menejimenti na Viongozi katika kuboresha Sekta ya Afya nchini



# Watahiniwa 3099 Wafanya Mtihani wa Usajili na Leseni Katika Vituo Vinne



*Watahiniwa wa Mtihani wa Usajili na Leseni Kituo cha UDOM, wakisikiliza Maelekezo Siku moja kabla ya Mtihani*

*NA NDIMMYAKE MWAKAPISO*

Jumla ya watahiniwa 3099 ambao ni wauguzi na wakunga waliyohitimu katika vyuo mbalimbali Ndani na nje ya Tanzania, mnamo tarehe 23 Agosti 2024, wamefanya mtihani wa usajili na leseni ili kupata sifa ya kusajiliwa rasmi katika taaluma na Baraza la Uuguzi na Ukunga nchini kwa kutunukiwa cheti cha Baraza na Leseni zitakazowaruhusu kutoa huduma kwa jamii mara bada ya kufaulu mtihani huo wenye lengo la kupima umahiri katika taaluma.

Katika usajili wa watahiniwa ulioanza 01 Julai 2024 nakufungwa 14 Agosti 2024. Jumla ya watahiniwa 3,099 walikidhi vigezo na kusajiliwa kufanya mtihani, Watahiniwa hawa wanajumuisha ngazi ya Shahada 195, Stashahada 2823 na Astashahada 81.

Watahiniwa walikuwa wamegawanyika katika vituo vinne ambavyo ni;Chuo Kikuu cha Dodoma, UDOM kilichopo Jijini Dodoma, Taasisi ya Afya na Sayansi shrikishi Mbeya iliyopo katika Hospitali ya kanda Mbeya Jijini Mbeya, Chuo Kikuu cha Mt. Agustino (SAUT) kilichopo Malimbe Jijini Mwanza, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu (DUCE) kilichopo Temeke



Wakizungumza na TNMC Habari mara baada ya kutoka kwenye chumba cha Mtihani, baadhi ya watahiniwa waliopata fursa ya kuhojiwa ambao ni Willison Haule, Ramadhani William, wamesema, mtihani huo ulikuwa wa kiwango cha kawaida na umegusa maeneo yote muhimu ya kupima umahiri na weledi kwa ujumla na kusisitiza kuwa haukuwa mtihani mgumu kwa mtahiniwa ambaye alizingatia mafunzo kwa vitendo akiwa Chuoni.

Akitoa tathimini baada ya mtihani, msimamizi kiongozi wa kituo cha Chuo Kikuu cha UDOM Bi. Safina Mvungi, ambaye pia ni Afisa Muuguzi Mkufunzi amesema, zoezi la Mtihani huo lilienda vizuri na hakukuwa na changamoto yoyote iliyokuwa imejitokeza kwani watahiniwa wote walizingatia maelekezo na kufanya mtihani kwa utulivu.

Awali siku moja kabla ya mtihani walipata fursa ya kupata maelekezo muhimu ya mtihani, kukagua kumbi zilizotumika kufanyia Mtihani na kuona sehemu za kuketi kwa ajili ya mtihani.

Aidha, watahiniwa wanaofaulu mtihani huu ndio ambao hutambuliwa rasmi kama wataalamu wa kada ya uuguzi na ukunga na hupewa leseni na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ambayo huwaruhusu kutoa huduma kwa jamii.

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# Msajili TNMC: Mkazingatie Maadili ya Taaluma ya Uuguzi na Ukunga.



Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi.Agnes Mtawa akihutubia wakati wa katika Mahafali ya 50 ya kitaaluma kwa wauguzi na wakunga wanafunzi wa Chuo cha Sayansi Shirikishi Dodoma Agosti 2,2024.

**Na Ezekiel Nyalusi**

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agnes Mtawa, amewataka wahitimu wote wa kada ya Uuguzi na Ukunga hapa nchini, kuzingatia maadili ya taaluma yao hata baadaya ya kuhitimu vyuo vya kada hiyo.

***"Sensa ya mwaka 2022 inaonesha tuna watu zaidi ya millioni 60 na hawa wote wanahitaji huduma za Afya kwa nyakati tofauti, ninyi mnapohitimu leo jamii inategemea huduma bora kutoka kwenu, labda niseme kwamba Wananchi wanapokuja katika maeneo ya kupata huduma wanachohitaji ni huduma bora na salama kutoka kwa mtaalamu aliyeiva, hata hivi vyeo tunavyoitana wao hawavijui wao wanatarajia huduma bora, sasa niwaase mtakapoenda kuhudumia jamii mkazingatie maadili, nidhamu na weledi mlioupata kwa muda wa miaka mitatu."***
**-Msajili TNMC**

Msajili ameyasema hayo wakati akihutubia kama mgeni rasmi katika Mahafali ya 50 ya kitaaluma kwa wauguzi na wakunga wanafunzi wa Chuo cha Sayansi Shirikishi Dodoma Agosti 2,2024.

Katika hatua nyingine Msajili aliwakumbusha wanataaluma hao kuifahamu na kuiishi misingi saba ya Maadili ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga hapa Nchini.

***"Najua darasani mmejifunza mambo mengi nataka niwakumbushe hili katika taaluma ya Uuguzi na Ukunga tuna Misingi saba ya maadili ya kitaaluma ambayo ni lazima yazingatiwe na wauguzi na wakunga watarajiwa misingi hiyo ni kama ifuatavyo: kuthamini utu na Maisha ya Mtu, lazima upate ridhaa ya mpokea huduma kabla hujatoa huduma, uwajibikaji wa kile unachokifanya, kufanya kazi kwa kushirikiana na wanataaluma wengine, kuwa mwaminifu na kutoa huduma bila upendeleo, Kutunza siri za Mteja pamoja na kujiendeleza kitaaluma."***
**-Msajili TNMC**





Naye Kaimu mkuu wa wa chuo Bi. Beatrice Kambuga, amemshukuru msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Bi. Agnes Mtawa, kwa kukubali kuwa mgeni Rasmi katika Mahafali hayo huku akiwataka watahiniwa hao kujiandaa vyema na mtihani wa utamilifu uliopo mbele yao sambamba na kujinoa kuelekea mtihani wa usajili na leseni unaoandaliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Katika Mahafali hayo jumla ya watahiniwa 105 wa ngazi ya stashahada katika taaluma ya uuguzi na ukunga, walitunukiwa vyeti vya kuhitimu masomo yao.

# Wizara ya Afya na Taasisi zake zatwaa Tuzo Maonesho ya Nanenane Jijini Dodoma.



**Na Mwandishi wetu**

Wizara ya Afya na Taasisi zake ambazo ni pamoja na Baraza la uuguzi na ukunga Tanzania TMNC, imetwaa tuzo ya mshindi wa tatu kati ya Wizara Mtambuka lizoshiriki Maonesho ya Kimataifa ya Nanenane yaliyoanza 01-10 Agosti 2024 Jijini Dodoma.

Tuzo hiyo ambayo imetolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan, imekabidhiwa siku moja kabla yakukamilika kwa Maonesho hayo Agosti 10, 2024.




Wizara ya Afya pamoja na Taasisi zake imetunukiwa tuzo hiyo kwa kuwa miongoni mwa Wizara Mtambuka zilizotoa huduma kwa Ubora katika kipindi chote cha Siku kumi za maonesho, ambapo zaidi ya wananchi wasiopungua 10,000 wametembelea Mabanda ya Wizara na kupatiwa huduma.

Baadhi ya huduma zilizokuwa zikitolewa katika viwanja vya maonesho ni pamoja na uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi, chanjo ya homa ya Ini na UVIKO-19, Elimu juu ya Afya ya akili, upimaji wa VVU/UKIMWI,upimaji wa kifua kikuu (TB), Maleria pamoja na, Elimu kuhusu Tiba Asili na Elimu juu ya Lishe.

Aidha, Baraza la Uuguzi na Ukunga (TNMC) limekuwa miongoni mwa taasisi za Afya zilizoshiriki maonesho hayo ya kitaifa yaliyofanyika jijini Dodoma likijikita katika utoaji wa elimu juu ya majukumu yanayotekelezwa na Baraza sambamba na zoezi la uhuishaji wa leseni pamoja na majukumu yote yanayotekelezwa na Baraza kwa wauguzi na wakunga.




Maadhimisho ya sherehe za Nanenane mwaka huu zimebebwa na kali mbiu isemayo ***"Chagua Viongozi Bora wa Serikali ya Mtaa kwa Maendeleo Endelevu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi"*.**



# Baraza la Uuguzi na Ukuguzi, Baraza ya Madaktari Yatakiwa Kutumia Mifumo

**Na Mwandishi Wetu**

Mwenyekiti Kamati ya kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI Mhe. Elibariki Kingu (MB), amelitaka Baraza la Uuguzi na Ukunga pamoja na Baraza la Madakatari Tanganyika(MCT) kuanza kutumia mifumo ya kieletroniki ili kupunguza gharama na kuboresha huduma za usimamizi wa mabaraza hayo.

Mhe. Kingu amesema hayo Agosti 14, 2024 kwenye kikao cha kamati ya kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI kilichofanyika ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma baada ya wasilisho la taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Uuguzi na Ukunga pamoja na Baraza la Madaktari Tanganyika.

***"Mabaraza haya yanafanya kazi kubwa ya kuhakikisha weledi wa kazi na taaluma unaimarika, asilimia kubwa ya Watanzania wanapata huduma kupitia watumishi wa Sekta ya Afya ambao wanatakiwa kupitia kwenye mabaraza haya, ni muhimu kuweka mifumo yenu ya kielectroniki vizuri ili kupunguza gharama na kuboresha huduma hizi kwa wauguzi na wakunga, pamoja na madakatari"*** amesema Mhe. Kingu






Wakati huo huo Mheshimiwa Kingu ameielekeza Wizara ya Afya kuendelea kuboresha mabaraza hayo kwa kuwa na mabaraza machache yenye ufanisi na tija pamoja na kuongeza rasilimali watu ili kupunguza uhaba wa wataalamu kwenye Sekta ya Afya.

***"Tuwapongeze kwa Mawasilisho mliotoa, yametupa uelewa mpana kuhusu namna Mabaraza yanavyofanya kazi lakini pia tumeona kuna uhitaji mkubwa wa taalamu kutokana na wasilisho hilo ambalo lina onesha kuwa bado wahudumu hawatoshi."*** Amesema Mhe. Kingu

Mhe. Kingu ametumia fursa hiyo kuyapongeza mabaraza yote mawili kwa namna yanavyo fuatilia kwa undani wataalam na kusimamia miiko na maadili pamoja na utaalamu na ubingwa bobevu.

***"Sasa tumeelewa ni kwa namna gani wataalam wanapatikana, tuwapongeze tu kwa namna mnavyoendesha na ufatilia wataalam kabla ya kuwasajili na kuwapa leseni, hii itasaidia katika kutoa huduma tena zinazokidhi ubora kulingana na viwango vilivyopo."*** Alihitimisha Mhe. Kingu.




@tnmchabari www.tnmc.go.tz



# Wauguzi, Wakunga 6,000 Watakiwa Kuhuisha Leseni Zao

Na Mwandishi Wetu



Mkurugenzi wa Usajili, Leseni na Maadili Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) Bi. Jane Mazigo, amesema zaidi ya wauguzi na wakunga 6,000 wanatakiwa kuhuisha leseni zao ifikapo Disemba 30.2024 ili waendelee kuwa na sifa ya kutoa huduma za Uuguzi na Ukunga hapa nchini.

***"Napenda kuwafahamisha wauguzi na wakunga wenzangu kuwa dirisha la kuhuisha leseni limefunguliwa tangu tarehe mosi mwezi wa saba 01/07/2024 na litaendelea kuwa wazi hadi tarehe 30 Disemba 2024 ambapo katika kipindi hiki Baraza litapokea maombi ya kuhuisha leseni kwa mujibu wa miongozo na ifikapo tarehe 01/01/2025 malipo hayo yataambatana na faini"*** - Bi. Mazigo

Mkurugenzi Bi. Mazigo, ameimbia TNMC Habari kuwa, uhuishaji wa leseni zinazowaruhusu wauguzi na wakunga kutoa huduma hapa nchini ni kwa mujibu wa Sheria namba moja ya Uuguzi na Ukunga iliyotungwa na Bunge mwaka 2010 pamoja kanuni zake ambapo kifungu cha 21(1) cha Sheria hiyo kinaelekeza kwamba Msajili atatoa leseni kwa Muuguzi au Mkunga ambaye amesajiliwa au kuorodheshwa ili kumruhusu kutoa huduna za Uuguzi na Ukunga nchini.

Aidha, kifungu cha 38(1) kimeainisha adhabu dhidi ya Muuguzi au Mkunga atakayebainika kutoa huduma kinyume na Sheria hii, ambapo adhabu yake ni kifungo cha muda usiozidi miaka mitano au faini isiyopungua shilingi milioni moja au isiyozidi shilingi milioni tano au vyote kwa pamoja.

Hivyo, amewataka wauguzi na wakunga wote ambao leseni zao zimekwisha muda wake, wanatakiwa kuhuisha leseni zao ili kutii Sheria halali inayotoa mwongozo wa namna ya uendeshaji na usimamizi wa taaluma ya Uuguzi na Ukunga hapa nchini.

Bi. Mazigo, ameendelea kuwasisitiza wauguzi na wakunga kufanya uhuishaji kwa wakati na kuzingatia sharti muhimu ambalo humtaka kila muuguzi au mkunga awe amepata au amehudhuria mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma yaani Continuing Professional Development (CPD) kabla ya kuhuisha leseni yake kwa lengo la kupata ujuzi na maarifa mapya yanayosaidia katika kuboresha utoaji huduma za Uuguzi na Ukunga na akatanabaisha kuwa leseni zote zinahuishwa kupitia mfumo rasmi wa Baraza ***https://tnmcis.tnmc.go.tz*** .




Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# HABARI PICHA



Wahitimu katika Mahafali ya 50 ya kitaaluma kwa wauguzi na wakunga wanafunzi wa Chuo cha Sayansi Shirikishi Dodoma Agosti 2,2024



Mtaalamu wa saikolojia Joeli nanauka akipata maelekezo juu ya majukumu ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania wakati wa Maonesho ya ya kimataifa ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Dodoma.



Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama(wa tatu kulia ) akikabidhiwa rasmi ofisi na aliyekuwa Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu (wa pili kulia



Afisa wa TNMC akizungumza jambo na wanafunzi wa shule ya sekondari waliofika katika Banda la Maonesho ya kitaifa ya Nanenane - Dodoma kufahamu majukumu ya Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.



Msajili TNMC (wa kwanza kushoto) akizungumza jambo na Afisa wa TNMC alipotembelea Banda la TNMC katika Maonesho ya kimataifa ya Nanenane yaliyofanyika Jijini Dodoma.



Msajili TNMC (wa kwanza kushoto) katika Mahafali ya 50 ya kitaaluma kwa wauguzi na wakunga wanafunzi wa Chuo cha Sayansi Shirikishi Dodoma Agosti 2,2024

# TNMC Yashiriki Kikao Kazi cha Msajili wa Hazina Jijini Arusha

**Na Mwandishi Wetu**



Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)Bi. Agnes Mtawa, ameshiriki kiako cha wakuu wa taasisi za Serikali, mashirika ya umma na wenyeviti wa bodi, ulioandaliwa na ofisi ya msajili wa hazina Jijini Arusha kuanzia tarehe 27 -30 Agosti 2024.

Mashirika ya Umma yapatayo 248 na Mashirika yasiyo ya Umma 58 kupitia kwa Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu yamekutana jijini Arusha katika Kikao cha Pili cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu kilichoandaliwa na Msajili wa Hazina.

Akizungumza katika kiakao hicho Msajili wa Hazina Bw. Nehemiah Mchechu amesema Mwaka huu Kikao hicho kinajikita katika kuzisukuma Taasisi na Mashirika ya Umma kufikiria ili kuweza kuwekeza nje ya nchi ili kuleta maendeleo endelevu nchini.

Amesema Uwekezaji huo nje ya nchi utasaidia nchi kuutawala uchumi hivyo hakuna sababu ya Taasisi za Umma kushindwa kuwekeza nje ya nchi kutokana na ukweli kuwa baadhi ya huduma zinagusa wateja walio nje ya mipaka ya ya Tanzania.

Amesema ili kufanikisha suala la Uwekezaji nje ya nchi, utendaji wa kazi wa Taasisi za Umma unapaswa kubadilika ili kuwa na mawazo mapana yatakaziwezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kupata matokeo chanya.
Ameongeza kuwa Taasisi zinapaswa kuwa na mipango ya muda mrefu ili ziweze kuchangia kwenye Mpango Mkakati wa Nchi wa Mwaka 2025 na hawapaswi kusubiri Tume ya Mipango zifanye zenyewe.



# TANZIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga limepokea kwa masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele za haki Mwezi Agosti, 2024, baada ya kumaliza kazi yao hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao mahali pema Peponi AMENI.



**JINA: ZEBEDEO E. MSIGWA**
**KITUO :** Hospitall ya Rufaa Songea.
**MKOA :** Ruvuma
**WILAYA :** Songea



**JINA: AMINA A. MIKIDADI**
**KITUO :** Hospitall ya Rufaa Mara
**MKOA :** Mara
**WILAYA :** Bunda



**JINA: TUMAIN Z. OMARY**
**KITUO :** Hospitall ya Babati.
**MKOA :** Manyara
**WILAYA :** Babati.



**JINA: FLORA MASATU**
**KITUO:** Hospitall ya Rufaa Morogoro
**MKOA :** Morogoro
**WILAYA :** Morogoro



**JINA: PAUL KILAMILE**
**NGAZI :** Hospitall ya Rufaa Njombe
**MKOA :** Njombe
**WILAYA :** Njombe



**JINA: JANET J MOSHI**
**KITUO:** Mikocheni Dispensary
**MKOA :** Kilimanjaro
**WILAYA :** Moshi

# TANZIA

Inaendelea........



**JINA: PAULINE KASOYAGA**
**KITUO :** Mkuu wa Chuo cha Uuguzi na Ukunga
**CHUO :** Massana  Collage - Dar es salaam

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA




# MTIHANI MWEMA DARASA LA SABA

Baraza la Uuguzi na Ukunga linawatakia Mtihani Mwema wa Taifa  Darasa la Saba 2024, Wanafunzi wote  wanaotarajia kuanza  tarehe 11-12 Septemba.

---

@tnmchabari    www.tnmc.go.tz

# JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu:0737-96-26-91**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA